Title: DRC: Band **Staff Benda Bilili**
Author: Saleh Mwanamilongo
Editor: Josephat Charo
Translator: Zainab Aziz
Proofreading: Tony Dunham
Sound Clips DALET: Learning by Ear: PEO_DRC_xxx

If you want to use additional music, here it is: DALET: Learning by Ear: PEO_DRC_00_SFX Additional Music

---

**Characters:**

1 Narrator, male or female voice

Voice-overs

Roger Landu, male, 18

Papy Manzambi, male

Jean Claude Bofondo, male

Vincent Kenis, male

Ricky Likabu, male

**INTRO**

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga maisha Yako. Kipindi chetu leo kinahusu watu wanaoleta mabadiliko. Leo hii tunaangazia mchango mkubwa wa kijana mwenye ulemavu na jinsi anavyotumia kipawa chake cha muziki kuiburudisha jamii na wakati huo huo kuielimisha jamii hiyo. Bila shaka msikilizaji ungependa sana kujua zaidi kuhusu kijana huyu. Nami bila kupoteza muda

nakukaribisha tuandamane pamoja hadi huko Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo!

1. **SFX Song Staff Bilili**

2. **Narrator**

Bendi ya muziki ya STAFF BENDA BILILI, ina makao yake jijini Kinshasa, katika Jamuhuri ya kidemokrasia ya Kongo. Kundi hili lina wanamuziki 12, na wote ni walemavu. Vijana hao walemavu walipatwa na ugonjwa unaosabishwa na virusi vinayojulikana kwa kimombo Poliomelitis, virusi ambavyo husababisha ugonjwa wa kupooza yaani Polio. Baadhi ya vijana hao walemavu wanatumia viti vya magurudumu, na wengine wanatumia magongo. Leo katika kipindi hiki tunamzungumzia kijana Roger Landu mwenye umri wa miaka 18. Roger Landu ndie mdogo kiumri katika kundi zima la wanamuziki wa STAFF BENDA BALILI. Kiti chake cha magurudumu kimepakwa rangi ya kijani na kupambwa kwa macho madogo ya paka yaliyochorwa nyuma ya kiti hicho. Roger Landu alifukuzwa kutoka nyumbani kwao alipokuwa na umri wa miaka 12 na hapo ndipo kijana huyo alipoanza kurandaranda katika barabara za jiji la Kinshasa. Aliishi katika hali ya kurandaranda mabarabarani kwa muda wa miaka 6 hadi alipojiunga na kundi la muziki la Staff Benda Bilili.

### 3. Soundbyte Roger Landu 1 (Lingala)

*“Kusema kweli, nilikuwa mtoto aliyeishi mabarabarani bila matunzo yoyote. Nililala nje, nilizurura mjini na kwenye maeneo yaliyokuwa na watu wengi niliwatumbuiza watu hao kwa zeze langu, na hivyo niliweza kupata fedha kidogo. Wakati mwingine nilijiunga na kundi langu na tulicheza muziki pamoja. Lakini wakati wote nilioishi kiholela, sikuwahi kuiba kitu chochote kutoka kwa mtu yeyote. Wanamuziki maarufu wa nchini mwangu walinivutia sana na wakati wote walikuwa ni mfano wa kuigwa kwangu yaani nilitamani sana kucheza muziki kama wao.”*

### 4. Narrator

Vyombo vya muziki vinazyotumiwa na wanamuziki wa kundi la Staff Benda Bilili ni vyombo vya kiasili, wamevitengeneza wenyewe, kwa mfano kijana Roger ametengeneza kifaa chake kwa kutumia ngozi. Chombo hicho kikipigwa kinatoa sauti mfano kama zeze.

### 5. SFX Song of Satonge:

Kifaa hicho cha muziki amekipa jina la ´SATONGE´

### 6. Soundbyte Roger Landu 2 (Lingala)

*“Kifaa changu hiki kinafanana na gita la kwanza yaani lead guitar, lakini sio gita hasa. Kifaa hiki kinaitwa SATONGE. Nilitumia fito, Kopo la nyanya na usinga. Nilitengeneza kifaa hiki miaka kumi iliyopita. Nafikiri katika siku za usoni nitakuwa mtaalamu wa gita la kamba moja la SATONGE ”.*

7. **Narrator**

Roger anasema kuwa kifaa chake hicho cha SATONGE kimemfanya awe maarufu, hasa katika kundi lake la - Staff Benda Bilili. Wanamuziki wenzake wanamuhusudu sana kutokana na kipaji chake cha kucheza kifaa hicho. Roger anakumbuka jinsi mama yake alivyokuwa anamkemea utotoni mwake kila alipokuwa akiimba na kukicheza chombo chake hicho cha SATONGE.

8. **Soundbyte Roger Landu 3 (LINGALA)**

*"Satonge ni chombo cha kienyeji cha kiafrika na bado hakijulikani kwenye muziki wa kisasa. Mimi ndie wa kwanza kukitambulisha chombo hiki cha SATONGE. Nilianza kukicheza kifaa hiki tangu nilipokuwa na umri wa miaka 9. Mama yangu alinikaripia sana kila siku kwa sababu yeye hakupenda kuniona nikibobea kwenye shughuli za kuimba katika umri ule mdogo. Lakini mimi niligoma katakata na nikazidi kusonga mbele na ndoto yangu ya kuwa mwanamuziki kwa hivyo niliendelea kuimba na rafiki zangu, wakati ule nilidhani labda niliyafanya hayo kwa sababu ya utoto lakini wapi mpaka leo bado niko hivyo hivyo. Hivi sasa nimefanikiwa kurekodi nyimbo kadhaa kwa kutumia chombo changu hiki cha SATONGE"*

9. **Narrator**

Staff Benda Bilili ni kundi la muziki ambalo limebahatika kuugusa na kuukonga moyo wa bwana Vincent Kenis, Mtayarishaji wa muziki mwenye asili ya Kibelgiji. Kenis alihusika sana katika kutayarisha na

kurekodi Albamu ya kwanza ya kundi hili la Staff Benda Bilili. Yeye alitambua kutoka mwanzo kipaji maalumu walichonacho wanamuziki kutoka Kongo.

**10. Soundbyte Vincent Kenis (French)**

*´´Kundi la muziki la - Staff Benda Bilili – limenivutia sana hasa kwa sababu ya mtindo wao wa Rumba ambao umechanganyika na madoido mengine. Yaani muziki wao ni mzuri kweli. Tena muziki wao wa kipekee kwa sababu wanatumia vyombo vya aina yake pia. Kwa mfano huyu kijana Roger, ambae anacheza chombo ambacho mimi mwenyewe nilikiboresha sauti yake. Chombo hiki cha SATONGE kinasikika kama vile gita la umeme na kinatoa sauti kama vile ya muziki wa rock. Lakini ukikiangalia vyema chombo hiki, sio gita hata kidogo. Watu wanapendezwa sana na sauti ya chombo hiki."*

**11. Narrator**

Licha ya kujiunga na kundi hili la muziki la Benda Bilili na kuendelea kutumbuiza mabarabarani, mafanikio ya kundi hili ni machache na maisha ya kijana - Roger Landu bado hayaridhishi, kifedha na hali ya maisha yake kwa jumla. Juu ya hayo yote kijana huyu hajidunishi kwa kuombaomba kama ilivyokuwa hapo awali alipoishi kama mtoto wa mitaani. Kijana Roger anathamini pato lake dogo analopata kutoka kwa watu wanaopendelea kukisikiliza chombo cha SATONGE :

**12. Soundbyte Roger Landu (Lingala)**

*"Wakati wowote mtu anaponipa fedha basi mimi humchezea muziki. Awali sikuweza kutafakari jinsi chombo changu hiki cha Satonge kilivyo muhimu. Kila niendapo nakibeba chombo changu. Nimekuwa mtu maarufu kwa sababu ya hii Satonge. Kusema kweli chombo hiki ndicho kilichonikutanisha na mtayarishi wa muziki wa kundi langu la Benda Bilili - huyo bwana ni Mfaransa anaitwa RENAUT. Yeye ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kuvutiwa na chombo changu na hapo ndipo alipoamua kunitambulisha kwenye bendi ya Staff Benda Bilili. Sasa nina muda wa miaka mitano kwenye kundi hili la muziki pamoja na kuwa mimi ni mlemavu."*

**13. Narrator**

Maisha ya kundi zima la Staff BENDA BILILI bado yanakabiliwa na panda shuka nyingi. Kila jioni kundi hili linatumbuiza kutoka mkahawa mmoja au baa moja hadi nyingine kwa malipo duni kama anavyoeleza kiongozi wa kundi hili la Staff Benda Bilili Jean Claude BOFANDO.

**14. Soundbyte Jean Claude BOFANDO (French)**

*"Sio mimi peke yangu bali kundi zima hili linakabiliwa na matatizo kadha wa kadha katika maisha yetu. Hii ni kwa sababu kwanza hatuna makao. Wengine wetu hulala kijuu juu tu mjini, wengine wanalala kwenye sehemu za kuwahifadhi walemavu au hata kwenye nyumba za mayatima. Kusema kweli maisha yetu hayaridhishi hata kidogo, hatujui hata jinsi ya kukimu mahitaji ya watoto wetu. Lakini*

*tunajitahidi kadri ya uwezo wetu. Hatutaki kufa na njaa, humu nchini mwetu, eti kwa sababu sisi ni walemavu! Hatutaki hata kidogo."*

**15. Narrator**

Hali halisi ya walemavu nchini Kongo ni ngumu. Roger na rafiki zake hawana uwezo wa kufanya kazi nzito za mikono. Hawana bima ya afya. Kwa hivyo walijiamulia kukimu maisha yao kwa kucheza muziki. Wameamua hivyo ili kuwa mfano wa kuigwa na walemavu wengine na pia kuielimisha jamii kuhusu ugonjwa wa Polio, kundi la Staff BENDA BILILI tayari limeshatunga wimbo kuhusu ugonjwa huo. Kampeni dhidi ya ugonjwa huu wa Polio ni muhimu. Mwaka uliopita katika Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo ilianzishwa kampeni ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa Polio baada ya ishara za kuenea kwa ugonjwa huo kujitokeza. Awali ilidhaniwa kuwa labda ugonjwa huo ulikuwa umetokomezwa kabisa nchini kote. Wimbo wa kundi la Benda Bilili unawahimiza wazazi kuhakikisha kuwa watoto wao wamepata chanjo dhidi ya Polio.

**16. SFX Staff Benda Bilili - POLIO Song**

**17. Narrator**

Wazazi wengi wameitikia wito wa wimbo huo kuhusu Polio kwa kishindo. Mmoja kati ya wazazi hao ni, Papy MANZAMBI, ambae anaamini kuwa kundi hili la muziki linapaswa kuungwa mkono kutokana na kazi nzuri inayofaywa na wanamuziki hawa chipukizi.

**18. Soundbyte Papy Manzambi (French)**

*"Kilichonivutia zaidi ni aina ya muziki unaochezwa na vijana hawa. Muziki wao ni mzuri sana. Natoa mwito kwa watu wote wema wawasaidie vijana hawa kwa vyovyote vile itakavyowezekana. Ushauri wangu kwa watu wengine walio na ulemavu ni kwamba waige mfano wa - STAFF BENDA BILILI – vijana hawa wanafanya kazi kwa bidii kujikimu kimaisha licha ya kuwa wao ni walemavu."*

**19. Narrator**

Muziki umembadili kijana Roger Landu na kuwa mtu muhimu kwenye bendi yake – na zaidi kwenye familia yake. Awali, kwa sababu ya ulemavu wake, familia yake ilimfukuza kijana huyu kutoka nyumbani.

**20. Soundbyte Roger Landu (Lingala)**

*"Kwa sababu ya chombo changu na kazi yangu ya muziki, siku hizi jambo la kulala nje limegeuka kuwa ndoto ya zamani. Sasa nimejumuika tena na familia yangu. Ninajitahidi kuona kwamba maisha yangu yanaendelea vyema na familia yangu inapata mafanikio pia. Ninataka kumiliki makao yangu binafsi."*

**21. Narrator**

Kupitia muziki wao ambao unapendwa na wengi nchini Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, kundi la Staff Benda Bilili limedhihirisha wazi kuwa "Ulemavu Sio Kutokuwa na Uwezo" . Ndoto ya Roger Landu ni kuimarisha maisha ya familia yake kutegemea kazi yake ya Muziki.

**22. Soundbyte Roger Landu (Lingala)**

*"Matumaimi yangu sio kuwa fundi spana katika gereji ya kutengeneza magari, sio kuwa kibarua wa ujenzi au fundi seremala. Nimejitolea kwa moyo wangu wote katika fani ya muziki. Natumai nitapata umaarufu duniani kote."*

**23. Narrator**

Ndoto ya kijana Roger Landu ni sawa kabisa na ndoto waliyonayo wanachama wote 12 wa kundi la Staff Benda Bilili , Ricky LIKABU anaeleza zaidi.

**24. Soundbyte Ricky Likabu**

*"Sasa tunaendelea vyema na muziki wetu ambao tunatunga wenyewe. Awali tulikuwa tunacheza muziki wa kuiga kutoka kwa wanamuziki mbalimbali wa kimataifa. Tuna imani kubwa kuwa muelekeo tunaofuata ni sahihi."*

**25. Narrator**

Kundi la Staff Benda Bilili limejifungulia milago ya mafanikio kimataifa pamoja na wale wote ambao wananyanyapaaliwa kutokana na hali ya ulemavu . Roger Landu anatilia mkazo kuimarisha kipaji chake cha muziki na pia kuendeleza mchango wake katika jamii. Roger Landu kweli ni kioo cha jamii.

**26. SFX_01_SONG Staff Bilili**

**OUTRO**

Je, msikilizaji ni yapi maoni yako? Je, unamuona kijana Roger Landu kama kweli ni mfano wa kuigwa? Tutumie ujumbe wako. Kama ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao au kumwambia rafiki juu ya kipindi hiki, tembelea mtandao wetu, anuani ni kama ifuavyo: www.dw-world.de/lbe. Na mpaka hapo ndio tumekamilisha kipindi chetu kwa leo kuhusu watu wanaotoa michango mizuri mbalimbali yenye lengo la kubadili maisha ya wengine katika jamii yetu. Hadi tutakapokutana tena, Kwaheri.

**END**